KIDATO CHA NNE KAZI YA ZIADA/KUDURUSU

1. Andika sentensi ifuatayo kwa wingi
   Uwanja mwingineo umechimbuliwa kuongeza ule wa zamani (alama 1)
2. Unda jina kutokana na kivumishi hiki
   (alama 1)
   Refu
3. Tunga sentensi tano tofauti kuonyesha matumizi tofauti ya kiambishi 'ki'
   (alama 5)
4. Tumia kitenzi 'kaa' inavyofaa kujazia nafasi zilizoachwa
5. Tunga Sentensi tano kuonyesha matumizi matano tofauti ya neno 'kwa'(alama 5)
6. Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi
   - Minghairi ya
   - Maadam (alama 2)
7. Ni mbinu gani za lugha zinazotumiwa katika sentensi hizi?
   - Juma ni simba wetu hapa kijijini
   - Juma ni shujaa kama simba (alama 2)
8. Sentensi ifuatayo ina maana mbili totauti. Zieleze
   Huyu amekuja kutuliza (alama 2)
9. Andika sentensi tatu kuonyesha maana tatu tofauti za neno KINA (alama 3)
10. Tofautisha maana
    - Ningekuwa na uwezo ningesafiri kwenda ng'ambo
    - Ningalikuwa na uwezo ningalisafiri kwenda ng'ambo
      (alama 2)
11. Yaandike maneno yafuatayo katika ufupi wake
    - Shangazi zako
    - Mama zako (alama 2)
12. Sahihisha makosa yaliyomo katika sentensi mbili zifuatazo
    - Bei za vitu zimepanda juu sana siku hizi
    - Weka mizigo kwa gari (alama 2)
12. Andika sentensi zifuatazo ukitumia kinyume cha neno lililoandikwa kwa herufi za

Mlazo

(i) Usijaribu *kupaaza* sauti unapoimba
(ii) Huyu ni mtu *mwenye busara*
(iii) Binadamu hawezi *kumuumbua* mwenzake

13. Akifisha kifungu kifuatacho

Bwana mwenyekiti wetu wa leo wazazi wote na hata wanafunzi leo ni siku muhimu je mngependa niwafahamishe msaada tuliopokea kutoka kwa wizara ya elimu
(alama 4)

14. Eleza matumizi ya 'Po' katika sentensi hii (alama 2)
    - Nilipofika nilimwona pale alipokuwa amesimama
15. Mtu akicheza mchezo mahali Fulani tunaweza kusema alichezea hapo
    - Ukifuata mfano huu, tumia vitenzi vilivyoko katika mabao kukamilisha
      (alama 2)

16. Andika katika msemo wa taarifa
Mzazi: Kesho nataka ufike nyumbani mapema, unasikia?
Mtoto: Nitajaribu, lakini mwalimu alisema tutafanya mtihani jioni (alama 4)

17. Badilisha katika udogo kasha uukanushe udogo huo
    - Guu lake limepona baada ya kuumwa na jibwa la jijini (alama 2)
    - Nyumba yenyewe ilijengwa bondeni karibu na mto (alama 2)
18. Andika katika kauli ya kutendesha
    - Nataka upike chakula hiki vizuri (alama 1)
    - Toa ushuru wa forodhani
19. Sahihisha bila kubadilisha maana:
    - Usikuje hapa kwetu kwani sitakuwamo (alama 1)
    - Basi la shule imeharibika moshi nyingi inatokea dirishani na maji inatiririka ovyo (alama 2)

20. Eleza matumizi manne tofauti ya – na (alama 4)
21. Eleza maana mbili mbili zinazotokana na sentensi zifuatazo
    (i) Mtoto alitimua mbio, kuona nyoka (alama 2)
    (ii) Juma alifagia chakula (alama 2)
    (iii) Sisikii vizuri (alama 2)
21. Bila kunyambua, andika maneno mawili ambayo yanatokana na shina moja na neno: imani (alama 2)
22. Changanua sentensi zifuatazo ukitumia michoro ya matawi, jedwali na mshale:

- Juma ameniletea kitabu ambacho nilikuwa nimekitafuta kwa muda mrefu.
- Nimemuona yule ninayemtafuta na neema zake.
- Ndoto zinazotisha ni za kishetani.
- Dadangu amefika nyumbani na kulala.
- Runinga ya Bwana Kazito imeharibika tena.
- Tulimwona nyoka mkubwa.
- Barua ilitumwa lakini haikumfikia Shakila.
- Mwalimu alikunja shati lake na kuwachapa wanafunzi kwa kiboko.
- Wote waliokufa watafufuka.
- Wanafunzi ambao hawatasoma vizuri wataanguka mtihani.

23. Ainisha shamirisho katika sentensi zifuatazo:

- Nyanya aliwasalimia wajukuu wake.
- Bustani la Kuzimu linawatisha watu wengi.
- Rita alimwandikia kakake barua kwa kalamu nyeusi.
- Mama aliwapikia watoto ugali tamu.
- Bibi anawasimulia wasichana wadogo hadithi za kikale.
- Rita alimwandikia kakake barua kwa kalamu nyeusi.
- Wetu wengine huvuna mahindi kwa panga.

- Mchungaji Thabiti alikufa kwa maji.
- Rita alimwandikia kakake barua kwa kalamu nyeusi.

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8 (a) Huku ukitoa mifano, fafanua majukumu **matano** ya nyimbo. (alama 10)

(b) "Mwimbaji ana nafasi muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa wimbo." Thibitisha. (alama 10)

Huku ukitoa mifano mwafaka, **linganisha** na **utofautishe** kipera cha vitendawili na kile cha methali. (alama 20)

9. Eleza maana ya malumbano ya utani. (alama 2)

Bainisha sifa **nne** za malumbano ya utani. (alama 8)

Fafanua majukumu **matano** ya malumbano ya utani katika jamii. (alama 10)

Eleza dhima ya Fasihi Simulizi. (alama 20)

10. Maigizo ni nini? (alama 2)

Tambua na kufafanua aina mbali mbali kuu za maigizo. (alama 4)

Eleza sifa nne za maigizo. (alama 8)

Ni upi umuhimu wa maigizo? (alama 6)

11. a) Umeanza mbinu na mikakati ya kukusanya na kuhifadhi Fasihi Simulizi. Taja sababu **sita** ambazo zinaweza kukupelekea kufanya hivi. (alama.6)

b) Taja matatizo **sita** ambayo unatarajia yakukabili katika shughuli hii (alama.6)

c) Je, jamii ya kileo inaendelezaje fasihi simulizi? Toa hoja **nne** na ufafanue. (alama 8)

KIGOGO

12. Thibitisha anwani ya Tamthilia Kigogo (alama 20)

13 Jadili mbinu anazotumia Majoka kuongoza Sagamoyo (alama 20)

14. “**Wasaliti nyinyi. Hamna shukrani hata!”**

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

b) Kwa nini mzungumzaji anaita wanozungumziwa wasaliti (alama 4)

c) Kauli hii imetawaliwa na kinaya. Thibitisha kwa kuchola mifano sita tamthliani (alama 12)

15. “Mwananmke ni nguzo muhimu katika ustawi wa jamii” Thibitisha (alama 20)

Mapenzi ya kifaurongo

“Wenye jadi kubeli wanapitia juu wachochole wanapitia chini ingawa wamo chuo kimoja na wanafanya masomo mamoja”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Eleza sifa mbili za anayehusishwa na kauli hii (alama 2)

c) Kwa kutoa mifano hadithini, thibitisha ambavyo wenye jadi kubeli wanapitia juu nao wenzao walalahoi wakipita chini (alama 14)

Shogake dada ana ndevu

Jadili jinsi suala la unafiki linajitokeza hadithini (alama 20)

Chozi la heri

Jadili maudhui tofauti katika riwaya ya ‘ chozi la heri’…… (kila maudhui alama 20)

Jadili mbinu mbalimbali za uandishi alizozitumia mwandishi kufanikisha kazi ya chozi la heri .